**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya simu: - **MKUU WA SHULE**
Simu: - 026 – 2782121
Namba ya mkononi **0769348479**
Email: njombehighschool@gmail.com
(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe
Kwa Mkuu wa Shule na sio mtu binafsi)
Unapojibu tafadhali taja: -
***KUMB. NA. NJS/J. I/6/2/VOL.II/121***

SHULE YA SEKONDARI NJOMBE,
S.L.P 144,
**NJOMBE**.
**24/04/2024**

Ndugu……………………………………
Mzazi/Mlezi………………………………
……………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano tahasusi ya ……………katika Shule ya Sekondari Njombe kwa mwaka wa masomo **2024/2025**. Shule ipo umbali wa kilometa tano kutoka stendi kuu ya Mkoa wa Njombe, usafiri wa Tax Tsh.7000/= na Pikipiki Tsh.3000/= toka kituo cha mabasi hadi shuleni.
Muhula wa masomo utaanza tarehe **______________** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **__________________.**

**2. KAULI MBIU YA SHULE "SCHOOL MOTTO" ELIMU NI UKOMBOZI.**
Kauli hiyo ndiyo itakuwa dira ya mwanafunzi wakati wote atakapokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili.Mwanafunzi anatakiwa kuitafakari kauli mbiu hiyo kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa Mwanafunzi atatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake na kwa Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, atatakiwa kuwa na tabia njema na ahudhurie masomo na kujifunza kwa bidii.

Tunakutakia safari njema.

Karibu sana

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NJOMBE
S.L.P 144 NJOMBE

**MKUU WA SHULE**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

### 2.2 MICHANGO YA SHULE

**(a) Michango mbalimbali: -**

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **jumla** | **80,000/=** |

Michango hiyo ilipwe kupitia akaunti namba **60610004040 NMB** jina la akaunti ni **NJOMBE SECONDARY SCHOOL**. Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye "pay in slip". Pindi afikapo shuleni aiwasilishe kwa Mhasibu wa shule.

**(b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni: -**

(i) **Ream za karatasi 2** kwa mwaka **(aina ya ream ni PAPERLINE)**
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa biology
(iv) Scientific calculator
(v) Godoro la futi $2^1/_2$
(vi) Mashuka pair 2 rangi ya blue, blanketi zito 1,mto na foronya 1, chandarua 1pembe nne.
(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(viii) Kila mwanafunzi aje na gumboot kwa ajili ya matumizi ya kazi za nje.
(ix) Kila mwanafunzi aje /awe na bima ya afya ni lazima

**SARE YA SHULE:**

- Suruali mbili (2) za Shule rangi ya dark blue zenye mifuko miwili (2) mbele na mmoja (1) nyuma. Upana miguuni inchi 18. Iwe na rinda mbili kila upande (dats)
- T- shirt (2) za dark blue zenye kola na zisizo na mchanganyiko wa rangi nyingine wala maandishi yoyote (Shamba dress)
- Sweta mbili (2) rangi ya "dark blue**.**"
- Njombe ni baridi sana mwanao aje na tracksuit nzito za kulalia rangi ya dark blue. Track isiwe na kofia.
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
- Tai dark blue ndefu moja
- Viatu vya ngozi vyeusi na visivyo na visigino virefu jozi mbili vya kufunga na kamba.
- Soksi jozi mbili nyeusi.
- Daruga au njumu na bukta za michezo
- Koti jeupe lenye mikono mirefu (Laboratory coat) kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi tu.
- Suruali za damu ya mzee mbili (2) za kitambaa, sare ya kazi za nje ya darasa mshono wa suruali: - iwe na mifuko mitatu, mmoja wa nyuma upande wa kulia na miwili mbele pande zote kulia na kushoto pembeni, iwe na rinda mbili kila upande upindo wa chini (Miguuni) ugeuzwe juu (turn up) Upana miguuni inchi 18 tu na si vinginevyo. **SURUALI ZA MITUMBA NA JEANS HAZIRUHUSIWI HAPA SHULENI**.

***Ili kuepuka kuingia gharama mara mbili kwa sababu ya kuchanganya rangi za Tshirt na sweta pamoja na suruali unashauriwa kuja kununulia vitu hivyo Njombe mjini baada ya kupewa maelezo ya rangi sahihi ya kitambaa na aina ya mshono unaokubalika hapa shuleni.***

**NB: -**

- ***Mwanafunzi anapokuja shuleni awe amevaa tracksuit rangi ya dark blue kama inavyoelekezwa hapo juu.***

- ***SIMU HAZIRUHUSIWI SHULENI, NI KOSA KWA MWANAFUNZI KUJA/KUMILIKI SIMU SHULENI MWANAFUNZI ASIJE NA SIMU KWA NAMNA YOYOTE ANAPO RIPOTI SHULE.***

**MASHARTI MENGINE:**

- ❖ Mwanafunzi asije shuleni na nguo nyingine zaidi ya zile alizoagizwa vinginevyo atarudishwa nyumbani.
- ❖ Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaoweza kutokea katika chumba chao. Uharibifu wowote ule ukitokea/ukibainika katika chumba kimoja wapo wanafunzi wanaoishi katika chumba hicho wataadhibiwa wote, kwani wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu wa mali ya umma. Mfano kuunganisha umeme kuchoma bweni, kuiba vitu. nk.
- ❖ Uharibifu wowote utakao sababishwa na mwanafunzi ni jukumu la mwanafunzi na mzazi/mlezi kugaramia matengenezo.

**VIFAA VYA JUMLA VINAVYOHITAJIKA NA KILA MWANAFUNZI SHULENI:**

Kutokana na uhaba wa vitendea kazi hapa shuleni mwanao aje na vifaa vifuatavyo:

i. CBG na PCB
Walete reki 1 na mpini wake, drier/squizer 1, Hard broom 1 na Toilet brush 1.

ii. PCM
Walete panga (skymark machete 204-16 **lililonolewa**) drier/squizer 1 na hard broom 1

iii. EGM NA HGK
Walete hard broom 1, panga (skymark machete 204-16 **lililonolewa**) moja gumu na imara na soft broom 1

iv. PGM NA HGE
walete soft broom, hard broom 1 na Ufagio wa kutolea buibui ukutani 1

v. HGL
Walete mopa na ndoo yake ya kudekia 1 na toilet brush 1

vi. HKL
Walete shoka kubwa ngumu iliyonolewa na Toilet Brush

vii. PMC
Walete jembe uma na mpini wake, drier/squizer 1 na hard broom 1

**NB; PAMOJA NA VIFAA VILIVYOAGIZWA HAPO JUU KWA KILA TAHASUSI: -**

- **Kila mwanafunzi anaporipoti shule aje na jembe lililonolewa Pamoja na mpini wake na kwanja mpya iliyonolewa.**
- Ndoo mbili (2) ndogo, moja kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe na nyingine kwa matumizi ya ofisi shuleni. Kwa wanafunzi wa kiislamu anatakiwa kuja na ndoo tatu, (3) ndoo mbili kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe na moja kwa matumizi ya ofisi shuleni.
- Madaftari makubwa kumi (10) aina ya "COUNTER BOOK" na kalamu za kutosha, mkebe na scientific calculator kwa wanafunzi wote, isipokuwa wanafunzi wa mchepuo wa HKL tu.
- Toilet papers za kutosha (12-15) kwa mhula mmoja.
- Vitabu vya masomo angalia orodha iliyoambatanishwa kwa kila somo.Anaweza kununua baadhi ya hivyo.

**MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI/MLEZI**

Maagizo yote ya fedha au mizigo vitumwe posta tu, ambapo muhudumu wa shule anaweza kuchukua na kuleta shuleni. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda kuchukua. Aidha taarifa nyingine inayomhusu mwanafunzi mfano taarifa ya kufiwa itumwe kwa Mkuu wa Shule na si kupitia kwa mwanafunzi. Taarifa kama hiyo haitasikilizwa.

**USAFI BINAFSI:**

Unatakiwa kuja shuleni na nywele fupi, usinyoe panki au upara, hairuhusiwi kufuga ndevu wala kucha. Aidha unatakiwa kuwa safi na uoge mara kwa mara.

**UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA USAFI:**

Unatakiwa utunze mazingira ya shule katika hali ya ubora na safi.

**USHIRIKI KAZI ZA MIKONO:**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza Elimu ya Kujitegemea pamoja na kuimarisha afya ya mwili.

**NIDHAMU:**

Ili uweze kujifunza na kufaulu katika masomo yako unatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria za shule zilizoambatanishwa nyuma ya fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani. Ni wajibu wako mzazi au mlezi.

**MICHEZO NA UTAMADUNI:**

Unatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mbali mbali mfano kuimba, kuigiza, skauti na kadhalika.

**DINI:**

Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani yake ili mradi shughuli hizo zinaendeshwa kufuata sheria za nchi na ratiba ya shule. Aidha mwanafunzi atasali/swali shuleni.

**KUTOKA NJE YA SHULE.**

Mwanafunzi ataruhusiwa kutoka nje ya shule mara moja tu kila Jumapili ya mwisho wa mwezi

**CHAKULA MAALUMU:**

Shule haitatoa chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine. Aidha mzazi/mlezi unashauriwa umtafutie mahali ambapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula kulingana na tatizo lake.

**NB: Hakikisha mara baada ya mwanafunzi kupokelewa akabidhi fomu iliyojazwa na daktari juu ya afya ya mtoto ofisi ya malezi**

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja NJOSS.

**Karibu sana.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NJOMBE
S.L.P 144 NJOMBE

**MKUU WA SHULE**

Nakala kwa:-

1. Katibu,
   Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
   S.L.P.1923
   **DODOMA.**

2. Katibu Tawala za Mkoa
   S.L.P. 668,
   **NJOMBE.**

3. Mkurugenzi Mtendaji,
   S.L.P.577
   **NJOMBE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI**

A. 1 . Jina la mwanafunzi………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………….
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya)………………………………(Mkoa)………………….
4. Dini…………………………… Dhehebu…………………………………………….

B: 1.Jina la Mzazi/Mlezi anayekutunza…………………………………………………..
2. Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………
3. Anuani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………
4. Mahali ambapo anaishi Mzazi/Mlezi……………………………………………….
Kijiji/Mji…………………………………..Kata……………………………………
5. Jina la anayekulipia Ada/Karo ya Shule……………………………………………..
6. Anuani yake…………………………………………………………………………....
7. Namba ya Simu…………………………………………………………………
8. Namba ya NIDA ya mzazi/mlezi ………………………………..
9. kopi ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.

**C:- Majina ya Ndugu wengine wawili wanao husika na malezi ya mwanafunzi huyo. Ingalifaa wawe**
**Wanaoishi Njombe au karibu na Njombe kwa ajili ya mawasiliano ya haraka.**

1. Ndugu……………………………………………………………………………….
   Anuani yake……………………………………………………………………………
   Namba ya Simu…………………………………………………………………………
2. Ndugu…………………………………………………………………………………
   Anuani yake…………………………………………………………………………..
   Namba ya simu……………………………………………………………………….

**D: Anuani za Ofisi ya Katibu Kata au Mwenyekiti wa Tawi/Kijiji ambako Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi anaishi**

1. **Jina la Katibu Kata……………………………………………………………………..**
   Kata ya……………………………………………………………………………..
   Anuani ……………………………………………………………………………..
   Namba ya Simu………………………………………………………………………
2. **Jina la Mwenyekiti wa Kijiji/Tawi……………………………………………………..**
   Kata ya ……………………………………………………………………………..
   Anuani ……………………………………………………………………………..
   Namba ya Simu……………………………………………………………………….

Zingatia: Tafadhali ijaze fomu hii kwa uangalifu

- Futa isiyohusika

**A: MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………………

Anuani…………………………………………………………………………………………..

Tarehe………………………………………………………………………………………….

Mimi……………………………………………………………………………………………
Jumuiya ya Shule ya Sekondari Njombe. Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu nitazingatia sheria na taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi ………………………………….Mzazi/Mlezi wa……………………………… nimesoma kwa makini maagizio ya shule yaliyotolewa yanayohumusu mtoto wangu. Ninakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Ninaahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………………….

Tarehe…………………………………………………………………………………………………
…..

**GOVERMENMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**The headmaster,**
**Njombe Secondary School,**
**P.O. Box 144,**
**NJOMBE.**

**Part A:-**
**To Medical Officer**

**………………………………**

**………………………………**

**Mr/Mrs/Miss……………………………………………………**
**(Name in Full)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time schooling course. The examinations should include the following categories (I – III) each category or sub – category of which will render the applicant in eligible in case of a defect.

I
a) Eye-Sight
b) Hearing
c) Limbs
d) Speech
e) Venereal Diseases
f) Leprosy
g) Epilepsy

II. Neuroses
III. Other serious diseases

Part B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be Completed by Government Medical Officer)

I have examined the above name and consider that he/she is physically fit/unfit mentally fit/unfit for a full-time schooling course.

(a) Eye-Sight…………….
(b) Hearing…………….
(c)Limbs…………..
(d)Speech………
e) Venereal diseases…………...
Leprosy…………….
Epilepsy…………………….
Neuroses……………
Other Series Diseases…………………………………………

Date……………………………………….. Signature……………………………………

Station……………………… …. Designation…………………………………

## ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

### A: HISTORY

1. Modern World History by Ben Walsh
2. African in the World History by Nyirenda
3. The Russian Revolution and the Bolshevik Victory by D.C. Heath and Company
4. Major events in the African history by Fr. Kamara.
5. Zamani East African History by B. Ogoti and J.A. Kieban
6. Essentials in Advanced Level Paper 1 & 2 by Salehe Yassin.
7. Advanced history for secondary schools forms five & six by Tanzania institute of education (T. I. E)

### B: ECONOMICS

1. Microeconomics for advanced secondary schools: students book form five & six (2022) by Tanzania institute of education (T. I. E)
2. Macroeconomics for advanced secondary schools: students book form five & six (2022) by Tanzania institute of education (T. I. E)
3. Essentials for A-level Economics paper 1 (form five and six) current syllabus (2018) by Ambrose Odhiambo 1st edition
4. Essentials for A-level Economics paper 2 (form five and six) current syllabus (2019) by Ambrose Odhiambo 1st edition

### C: PHYSICS

1. A -Level Physics by Roger Muncaster (fourth edition)
2. A -Level Physics by Roger nelkon and parker (7th edition)
3. A -Level Physics by Roger Tom Dimean (3rd edition)
4. Comprehensive Physics for A –Level
5. Physics for advanced level secondary schools form six (2019) by Tanzania institute of education (T. I. E)
6. Principles of physics for class xi (S'Chand & company PVT Ltd, new delhi)
7. Principles of physics for class xii (S'Chand & company PVT Ltd, new delhi)

### D: CHEMISTRY

1. Advanced Chemisrty Review by William W. Davis (Mzumbe book shop project, 2004)
2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe book shop project, 1998)
3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II. (Tanzania instate of education ,1995)
4. Organic Chemistry volume I. The Fundamental Princinples by I.L. Finar (Longman Ltd 1990)

### E: ADVANCED MATHEMATICS

1. Advanced Mathematics Vol. I By ministry of education and vocational training
2. Advanced Mathematics by shayo

3. Advanced Mathematics by Tranter and Laube
4. Pure Mathematics vol. I and II by Back House
5. Further Pure Mathematics by Bostock and Chandler Rourke
6. Advanced mathematics form V by P. L. Miyombya
7. Advanced mathematics form VI by P. L. Miyombya
8. Advanced mathematics form V by Tanzania institute of education (T. I. E)
9. Advanced mathematics form VI by Tanzania institute of education (T. I. E)
10. Scientific calculator f(x) = 991

**F. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic applied mathematics for form V and VI by Tanzania institute of education (T. I. E)
2. Scientific calculator f(x) = 991

**G. GENERAL STUDIES**

1. Mwaipaja M. (2018) General studies for form five and six
2. Kamili, Z (2017) General studies alive
3. Bigiriwamungu J. & Deogratias S. (2019) Understanding general studies
4. Stiftung, K. (2000) General studies: supplementary book for A-level and Colleges

**H: ENGLISH.**

1. English. for Advanced level by Dr. M. Kadeghe
2. Advanced English Dictionary –Oxford University
3. Selected poem from east Africa by TIE and others poems text books
4. I will marry when I want by Ngugi wa Thiong'o and other play/drama text books
5. His excellency the head of state by Danny Safo and other novels and short stories books
6. Betrayal in the city by Francis Imbuga
7. An enemy of the people by Henrick Ibsen
8. A man of the people by Chinua Achebe
9. The wonderful surgeon by Charles Mloka
10. The beautiful ones are not yet born
11. English for advanced secondary schools. Students book form five by Tanzania institute of education (T. I. E)
12. English for advanced secondary schools. Students book form six by Tanzania institute of education (T. I. E)
13. Advanced level English Language one Form five and Six by Shadrack and James Kinunda.

**I: KISWAHILI**

1. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee) DUP-DSM
2. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – TUKI.
3. Nadharia ya lugha kidato cha tano na sita na elimu ya juu (2016) na M. C. Saluhaya
4. Kiswahili 2 kidato cha tano na sita (2018) na Jonas Lwendo
5. Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA) sekondari na vyuo (2009) na Masamba na wenzake
6. Tahakiki ya Kiswahili 2

**J: GEOGRAPHY**

1. Practical geography for east Africa by D.M Sagata
2. Research methodology by C. R. Kothari
3. Practical geography for Africa by J. M. Pritchard
4. Human and economic geography by G. Morgan
5. Human geography by Tanzania institute if education (T. I. E)
6. Practical geography for advanced secondary schools Tanzania institute if education (T. I. E)
7. Physical geography for advanced secondary schools Tanzania institute if education (T. I. E)
8. Physical geography in diagrams 4th edition by R. B. Bunnett
9. Practical geography in diagrams by R. B. Bunnett

**K: BIOLOGY**

1. Rwehumbiza, R (2016). Complete advanced biology form five. TVTA Dar Es Salaam
2. Rwehumbiza, R (2016). Complete advanced biology form six. TVTA Dar Es Salaam
3. T. I. E (2019) Biology for Advanced level Secondary schools. Form Five. T. I. E Dar Es Salaam
4. T. I. E (2019) Biology for Advanced level Secondary schools. Form Six. T. I. E Dar Es Salaam
5. Taylor D. J, Green, N. P. O, Stout, G. W (1997) Biological science (3rd ed) Cambridge university press: U K
6. Toole, S. Toole, G (2014) Biology for advanced level (4th ED) Oxford University Press: Uk
7. Dissecting Kit.

**SHULE YA SEKONDARI NJOMBE**
**SHERIA ZA SHULE**

1. Wanafunzi wanatakiwa kusimama kumsalimu mtu yeyote anayewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano
2. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimiana na kuwa na ushirikiano
3. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu na kufanya kazi wanazopewa
4. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
5. Wanafunzi kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule
6. Wanafunzi waheshimu ofisi ya mkuu wa shule, ukumbi wa chakula, maktaba na madarasa.
7. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria masomo kwa wakati na kufanya mitihani yote inayomuhusu na kama kuna sababu ya kutohudhuria ielezwe mapema.
8. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria na kufanya kazi za mikono watakazopangiwa
9. Wanafunzi wanatakiwa kuwa katika mikusanyiko yeyote kama:- kupandisha bendera ya taifa ,baraza la shule,mikutano ya darasa na bweni.
10. Wanafunzi wanatakiwa kutii kengere kama mwito wa haraka
11. Wanafunzi wanatakiwa kuwa shuleni, shule inapofunguliwa kwa tarehe iliyopangwa.
12. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare ya shule:-
    (a) Darasani
    (b) Wanapotoka nje ya shule
    (c) Wakati wa baraza la shule
13. Wanafunzi watatoka nje ya shule kama wanashida binafsi kwa ruhusa ya :
    a) Mwalimu wa zamu na wanafunzi wanatakiwa kuwepo shuleni kabla ya saa12 jioni
    b) Ruhusa ya kulala nje ya shule inatolewa na mkuu wa shule tu.

**NB: Mwanafunzi akilala nje ya shule bila ruhusa atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe**

14. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine,sehemu hizi ni nje ya mipaka ya shule
15. Wanafunzi hawana ruhusa ya kuingiza mgeni yeyote bwenini au madarasani.
16. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo:-
    a) Vilabu vya pombe
    b) Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses)
    c) Nyumba za walimu/wafanyakazi wasio walimu ila kwa kibali maalumu tu.
17. Mwanafunzi anatakiwa kutunza:
    a. Mali ya umma kama madawati,vitanda,vifaa vya kulia,vioo vya madirisha,vitabu vifaa vya maabara na kadhalika
    b. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali binafsi
    c. Mwanafunzi anatakiwa kulala bwenini wakati wote wanapokuwa shuleni.
18. Wanafunzi wanatakiwa kuwa wasafi binafsi na kutunza mazingira
19. Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na jiko, heater na vifaa vingine vinavyotumia umeme.
20. ***SIMU HAZIRUHUSIWI SHULENI, NI KOSA KUMILIKI SIMU SHULENI.***

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi.
2. Uasherati.ubakaji na ushoga.
3. Ulevi wa pombe na madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi.
5. Kupigana au kumpiga mwalimu au mtumishi.
6. Kuoa.
7. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
8. Kutoa mimba /Kusaidia kutoa mimba.
9. Kutoa lugha chafu /matusi.
10. Kupatikana na makosa ya jinai.
11. Kugoma na kuchochea au kuongoza mgomo shuleni.
12. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
13. Kutohudhuria vipindi kwa muda wa miezi miwili bila sababu.
14. Kupatikana na simu au vifaa vyake.
15. Kutoroka mchana au usiku.
16. Kuchezea miundo mbinu mathalani ya umeme, maji, vyoo n.k.